


Hadithi ya Agostino

L'histoire d'Agostino



LIDA Italia 

Billie Cejka Risnes

 Jacob Haule

5 

 Kiswahili  / français 




LIDA Stories


lidastories.net

**Hadithi ya Agostino / L'histoire
d'Agostino**

LIDA Italia 

Billie Cejka Risnes

 Jacob Haule (sw), Zina (fr)



This work is licensed under a Creative Commons
[Attribution 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/4.0).
<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0>



Ninaitwa Agostino na nina umri wa miaka 51.
Kazi yangu ni kusambaza chakula kwa baiskeli.
Nina mabinti wawili, lakini ninaongea nao mara
chache sana. Mimi na mama yao hatuishi
pamoja tena kwa sababu tumeachana.


...


Je m'appelle Agostino et j'ai 51 ans. Mon travail
consiste à livrer de la nourriture à vélo. J'ai deux
filles, mais on se parle à peine. Leur mère et moi
ne vivons plus ensemble car nous avons divorcé.

Je vis avec ma mère, puisque je ne peux pas me permettre de payer un loyer après le divorce. Les loyers sont très chers dans cette ville.

...

Ninaishi na mama yangu kwa sababu siwezi kumudu kulipa kodi ya nyumba baada ya kuachana. Kodi ya nyumba ni gharama kubwa sana katika jiji hili.






Miezi michache iliyopita, nilikuwa nikifanya kazi kama bawabu katika kampuni. Nilitengeneza vitu vilivyoharibika, nilibeba maboksi, na nilimsaidia yeyote aliyehitaji msaada. Siku moja, kampuni ilinifukuza kazi. Sikujua ni kwa nini.

...


Il y a quelques mois, je travaillais comme agent d'entretien pour une entreprise. Je réparais ce qui était cassé, portais des cartons, et aidais ceux qui en avaient besoin. Un jour, l'entreprise m'a licencié. Je n'ai pas compris pourquoi.



Baada ya muda mrefu, jitihada zetu zikazaa matunda. Kampuni moja kubwa ya usambazaji ililazimika kulipa faini kubwa na kuwapa wafanyakazi wake ajira za kudumu. Ilikuwa ni mara ya kwanza jambo kama hili kutokea duniani. Inaonekana kama mambo yameshaanza kuboreshwa.

...


Après un long moment, tout notre dur travail a porté ses fruits. Une grande entreprise de livraison a dû payer une grosse amende et donner aux travailleurs des postes permanents. C'était la première fois que cela se produisait dans le monde. On dirait que les choses sont en train de s'améliorer.



Niliwaona watu wengi wakileta chakula kwa
baiskeli. Ninaweza kuendesha baiskeli, kwa hiyo
niligonga mlango wa kampuni kubwa ya
usambazaji. Walinipa yuro tatu kwa kila safari.
Ninaingiza yuro 40 kwa siku, yuro 60
nikibahatika sana, na wateja wananiongezea.

...

J'ai vu plein de personnes livrer de la nourriture
à vélo. Je peux faire du vélo, donc j'ai trappé à la
porte d'une grande compagnie de livraison. Ils
m'ont proposé trois euros par livraison. Je fais
40€ par jour, 60€ si j'ai beaucoup de chance et
que les clients me donnent des pourboires.



Kwa kushirikiana na madereva wengine wa
usambazaji kutoka katika makampuni mengine,
nilisoma kozi inayohusu haki za wafanyakazi
katika chama fulani nchini. Walitupa ushauri wa
kisheria bure kabisa. Tukapambana ili
tutambuilike na tupate haki zaidi.

...


Avec des livreurs d'autres entreprises, j'ai suivi
une formation sur les droits des travailleurs avec
une union locale. Ils nous ont proposé des
conseils juridiques sans aucun frais. Nous avons
des difficultés pour avoir plus de reconnaissance
et de droits.



Sipati likizo ya malipo, hakuna malipo ya kuugua, na haki mbalimbali kwa ujumla. Sidhani kama hii ni sawa, lakini ninahitaji kazi. Waajiriwa wengi ni wahamiaji kutoka sehemu mbalimbali duniani.

...

Je n'ai pas de congés payés, pas d'arrêts maladie payés, quasiment aucun droit. Je ne pense pas que cela est juste, mais j'ai besoin de ce travail. La plupart des autres employés sont des migrants du monde entier.



Watu wengi wanaofanya kazi ya usambazaji wanaumia katika ajali kila siku. Baadaye, wakati kijana wa miaka 25 anayefanya kazi hii alipogongwa na gari na akafa, mamlaka zikaanza kututambua. Ni aibu kwa sababu hili lilitokea baada ya yeye kufariki.

...

Beaucoup de livreurs sont blessés dans des accidents tous les jours. Puis, quand un livreur de 25 ans s'est fait renverser par une voiture et est mort, les autorités ont commencé à nous remarquer. C'est dommage qu'il ait dû mourir pour que cela se produise.